Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua

Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba sasa ya kwamba utapokea utukufu kutokana na kukusanyika kwetu pamoja. Tunakushukuru kwa ajili ya nafasi hii. Bariki Neno Lako linapotolewa kila usiku. Wabariki watu wako wanapolisikia. Na jalia Roho Mtakatifu mkuu alishike Neno linaloanguka moyoni, na kulifanya lijidhihirishe Lenyewe, kusudi hasa mamia ya watu, kote humu nchini, wapate kuokolewa. Mamia yao wanaoteseka, wanaokaa katika vivuli vya mauti, waweze kuona Nuru kuu ikichomoza, pia wapate kuponywa, na Jina Lako kuu litukuzwe. Hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa, Bwana, si kwa ajili ya kujiadhimisha wenyewe, bali kumtukuza Yesu Kristo miongoni mwetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

2 Sasa unapofungua Biblia yako, kwa dakika chache tu. Na kila usiku sasa nitazungumza tu kama dakika ishirini hadi thelathini. Nimekuwa nikifanya hivyo kwa majuma machache yaliyopita. Na nizungumze tu kwa dakika chache sana, na ndipo tutafanyiza mstari wa maombi, tuwaombee wagonjwa, ama chochote kile Roho Mtakatifu anachoongoza.

3 Na ni wangapi watakaoninii, mnaokuja kwa mara yenu ya kwanza usiku wa leo, na ninyi nyote pamoja, mtauombea mkutano, mtafanya hivyo? Sisi hatuko hapa kuninii tu . . . tuko—tuko hapa kwa sababu tunajaribu kusaidia. Ndugu, ninaamini, Bwana akitusaidia, tutakuwa na mkutano mkubwa kwa ajili ya kumtukuza Bwana na Mwokozi wetu.

4 Tunaamini Yeye yuaja, mara moja. Asipokuwa hapa usiku wa leo, nitakuwa nikimtarajia asubuhi. Asipokuwa hapa kesho usiku, nitakuwa hapa, Bwana akipenda. Halafu pia kama Yeye hayupo hapa, nitamtarajia kesho usiku. Halafu basi kama hayupo hapa, nitamtarajia usiku utakaofuata. Ninataka kufanya hivyo. Nimekuwa nikimtarajia kwa muda wa miaka thelathini na mitatu sasa, sehemu kubwa ya maisha yangu, wala sijakufa moyo. Ninamtarajia, kila siku, na kila saa, Yeye atokee.

5 Sasa tunapofungua katika Biblia, katika kitabu cha—cha Luka Mtakatifu, mlango wa 24, kuanzia kifungu cha 13. Na tusimame, kwa kuliheshimu Neno, tunaposoma. Luka Mtakatifu 24, kuanzia kifungu cha 13. Sasa kama wengine wenu mna Biblia zenu, wengine wao hupenda kuhifadhi somo la mhudumu, mahali anapozungumzia. Na sasa nitawataka msikilize kwa

makini. Someni pamoja nami kama mnaweza, kimoyomoyo, tunaposoma.

> *Na tazama, siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili.*
>
> *Nao walitembea pamoja . . . habari za mambo hayo yote yaliyotukia.* (Samahani.) *Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yote yaliyotukia.*
>
> *Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao.*
>
> *Macho yao yakafumbwa wasimtambue.*
>
> *Akawaambia, Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea, na mmekunja nyuso zenu?*
>
> *Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! Wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo . . . siku hizi?*
>
> *Akawauliza, Mambo gani? Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote;*
>
> . . . tena *jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulubisha.*
>
> *Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo;*
>
> *Naam, wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema,*
>
> *Wasiuone mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba wametokewa na malaika waliosema ya kwamba yu hai.*
>
> *Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikweda kaburini wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona.* Ndipo kasema . . .
>
> *Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!*
>
> *Je! haikumpasa Kristo kupata mateso haya na* kuingia *katika utukufu wake?*
>
> *Akaanza kutoka kwa Musa na manabii wote, akawaeleza . . . maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.*

Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele.

Wakamshawishi wakisema, kaa pamoja nasi, kwa kuwa kwaelekea *kuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao.*

Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.

Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.

Wakaambiana, Je! mioyo *yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia* maandiko?

Nao wakaondoka na wakaenda *saa ile ile, wakarejea Yerusalemu, wakawakuta wale kumi na mmoja wamekutanika, wao na wale waliokuwa pamoja nao,*

Wakisema, Bwana amefufuka kweli, naye amemtokea Simoni.

Nao waliwapa habari ya mambo yale ya njiani, na jinsi alivyotambulikana nao katika kuumega mkate.

6 Na tuinamishe vichwa vyetu. Bwana Yesu, tunaomba ya kwamba utajitambulisha kwetu namna hiyo, usiku wa leo, tunapokungojea. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

Mwaweza kuketi.

7 Kwa ajili ya somo kutokana na hayo, ningetaka kuchukua maneno haya: *Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua*.

8 Sasa tunazungumza, hasa, juu ya ufufuo, ambao unaaminiwa miongoni mwa Wakristo waaminio wote leo. Ndilo tumaini la Kanisa. Kama Kristo hakufufuka, basi tumepotea. Na Ukristo umewekewa msingi juu ya ufufuo, sasa, sio kibadala chake. Ufufuo! Kwa mfano, ufunguo huu wa moteli hapa, kama nikiuangusha huo sakafuni, na ningesema "Vema, niliuangusha, nitaubadili na mwingine unaofanana nao hapa," huo si ufufuo; hicho ni kibadala. Unaona? *Ufufuo* ni "kuinua kitu kile kile kilichoenda chini." Naye Mungu alimfufua katika siku ya tatu. Nasi tunaamini jambo hilo kwa moyo wetu wote, na tunaamini hadithi ya Biblia.

9 Pia angalia, katika asubuhi hii ya Pasaka ya kwanza, Yesu yu hai miongoni mwao, kutoka kwa wafu.

10 Ni jambo zuri jinsi gani! Jinsi nilivyo na furaha sana usiku wa leo kuitikia hilo kwa "amina," ya kwamba ninaamini Yeye angali hai miongoni mwetu, katika wakati wa kuchipuka kwa Injili tukufu ya Kristo. Ninaamini Yeye angali hai.

11 Ninaamini ya kwamba huo umekuwa ninii. . .Naam. Huo ulikuwa ni wakati wa kuchipuka kwa ufufuo, pia, kwa uhai, wa

mwanadamu. Mwanadamu daima aliogopa mauti; hawakuwa na uhakika wa kurudi tena kamwe baada ya kufa.

12 Lakini kumwona akifa pale Kalvari, kisha akifufuka tena na akawa pamoja nao, akitembea miongoni mwao katika siku hii tukufu. Baada ya kuhuzunika sana mioyoni na kusikitika, na kadhalika, walikokuwa wamepitia, na hizo saa zenye giza za kumwona Yeye akisulubishwa na kutemewa mate, na kudhihakiwa, na yote aliyokuwa amepitia katika miaka hiyo mitatu na nusu, na hizo saa za mwisho za giza zilizompata Yeye. . .Hao Mafarisayo, walimchukia, hata hivyo, nao walikuwa wakifurahi kwa sababu walidhani walikuwa wamemaliza jambo hilo, naye Huyu hapa anajitokeza kati yao! Jamani, ni siku ya jinsi gani! Ningeninii . . .

13 Hivi usingetaka kufanya safari pamoja na Kleopa na hao wengine, wakienda zao Emau? Ningalitaka kutembea pamoja nao. Na inawezekana. Ninafurahi kuwa hai leo, kwamba ningali ninaweza kufanya jambo lilo hilo, kutembea pamoja Naye leo jinsi tu walivyofanya wakati huo.

14 Wazo lenyewe, lilikuwa, jinsi ambavyo Yesu alikuwa amefufuka katika wafu. Lakini sehemu yake ya kuhuzunisha, ilikuwa, baadhi yao waliompenda, hawakujua jambo hilo.

15 Na hiyo hakika ndiyo picha ya siku hizi. Kuna watu wengi wanaompenda, ambao bado hawatambui ya kwamba Yeye yu hai. Wao, ni namna fulani ya historia ambayo wamejifunza katika shule fulani. Ni kitabu fulani cha theolojia, maadili fulani fulani, elimuadili, ambayo walisomea mahali fulani, na Yesu ni mtu wa kihistoria kwao. Na hata hivyo, katika historia, wanampenda, wala hawatambui ya kwamba Yeye yu hai pamoja nasi, akitembea moja kwa moja pamoja nasi, kama tu alivyofanya daima. Yeye yupo hapa vivyo hivyo tu kama—kama alivyopata kuwa.

16 Sasa, wao, sababu ya (wao) kwa nini hawakuamini jambo hilo, ni kwa sababu ule ufufuo ulikuwa si wa kawaida kabisa. Unaona, kulikuwako na . . .Jambo hilo halikuwa limetukia hapo kabla, kwa hiyo lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida kwao kuamini jambo kama hilo.

17 Na katika mambo yasiyo ya kawaida ndiko Mungu aliko. Mnaona? Kuzaliwa kwa Kristo kulikuwa si kwa kawaida, "bikira atachukua mimba." Mungu daima si wa kawaida. Yeye hufanya jambo lisilo la kawaida, bali daima ni kulingana na Neno Lake. Yeye kamwe hafanyi lolote nje ya Neno Lake, lisilo kawaida kabisa; kwa sababu, Yeye huliahidi kwanza, na kisha anamtuma mtu fulani kudhihirisha Neno hilo, kulifanya halisi kwa watu.

18 Wakati nyinyi Wapentekoste mlipoupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa mara ya kwanza, hilo lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida. Lakini hata hivyo Mungu aliahidi Hilo, "kummwaga

katika siku za mwisho," na likawa ndilo hili hapa. Kwa hiyo haidhuru lilikuwa lisilo la kawaida jinsi gani, ilikuwa ni ahadi ya Mungu ambayo ilipaswa kudhihirishwa, maana Mungu aliahidi.

19 Sasa ufufuo ulikuwa ni jambo lisilo la kawaida kwa nanii Wake wengi, watu waliompenda; hata hivyo ulikuwa ni Neno lililoahidiwa, ila lisilo la kawaida mno kuamini.

20 Uponyaji wa kiungu siku hizi, ni—ni jambo lisilo la kawaida sana kwa watu hata hawataki kuuamini, na hata hivyo ni Neno lililoahidiwa.

21 Jambo hili tunaloliona likitukia leo ni ahadi ya Mungu, lakini ni jambo lisilo la kawaida sana kwa moyo ambao haujapata kuwazia juu ya jambo hilo hivyo.

22 Na hivyo ndivyo ufufuo ulivyokuwa kwa watu wengi waliompenda. Kulikuwa na watu waliomheshimu na kumwamini kuwa ni nabii wa Mungu, na kumwamini Yeye kuwa Mwana wa Mungu, na kadhalika, lakini hata hivyo (wao, wao) u—ufufuo ulikuwa mgumu mno kwao kuuamini. Ulikuwa kitu cha ajabu mno.

23 Na ukichukua kitu chochote ambacho kweli ni cha ajabu namna hiyo, daima kichunguze kwa Neno. Na kama Neno lilikiahidi, basi ni Mungu tu akijitokeza jukwaani tena. Na hivyo ndivyo kila ahadi ilivyo.

24 Na hivyo ndivyo ilivyowapasa kuona jambo hilo wakati huo, maana Mungu aliahidi angemfufua katika siku ya tatu. Daudi alisema, "Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Yesu alisema, "Uharibuni mwili huu nami nitaufufua tena katika siku tatu." Unaona, ilikuwa ni ahadi.

25 Na lilikuwa ni jambo la ajabu sana, lisilo la kawaida kabisa, na wengi waliompenda hawakuweza kulielewa. Kwa sababu, lilikuwa—lilikuwa la kushangaza mno, kwa ulimwengu mzima, kwa mtu aliyekuwa amesulubishwa, na akachomwa upanga moyoni Mwake, ama mkuki, kila tone la damu mwilini Mwake lilikuwa limeisha msalabani, nao walikuwa wamemchukua na kumzibia kaburini, na kufingirisha jiwe juu yake, lililowachukua watu mia kulishughulikia, kisha kulitia muhuri kwa muhuri wa Kirumi, na kisha kusema, "Malaika alishuka na kuuvunja huo muhuri, kisha akalifingirisha hilo jiwe akaliondoa, Naye huyu hapa hai miongoni mwetu." Kwa namna fulani lilikuwa ni jambo geni.

26 Na leo hii ni ajabu ya namna iyo hiyo. Wakati watu wanapofikiri ya kwamba Yeye alikufa, hilo lilitosha, miaka elfu moja mia tisa iliyopita; na yupo hapa leo, baada ya miaka elfu moja na mia tisa, angali yuko miongoni mwetu, jinsi tu vile alivyokuwa wakati huo, dhahiri kabisa kama alivyokuwa wakati ule, akifanya mambo yale yale aliyofanya wakati huo. Ni ajabu kubwa mno. Watu hawawezi kulifahamu. Linapita fikira

zao. Hakika, ni nani anayeweza kumfahamu Mungu kwa akili? Hakuna mtu anayeweza kumfahamu Mungu kwa akili.

27 Hakuna mtu anayeweza kumfasiri Mungu. Mungu ndiye anayejifasiria. Mungu husema Neno; na watu husema, "Vema, una tafsiri mbaya." Mungu analifanya litimie, hiyo ndiyo fasiri. Hahitaji mtu yeyote kumfasiri. Ndiyo kwanza nizungumze juu ya jambo hilo, kwenye mji ulio chini ya huu. Mungu alisema, "Iwe nuru," na ikawa nuru. Halihitaji fasiri yoyote; kulikuwa na nuru. Mungu alisema "Bikira atachukua mimba," akachukua mimba. Hilo latosha. Kwa hiyo wakati anapozungumza jambo lolote, na basi Yeye—Yeye hujifasiria. Hahitaji fasiri zetu za jambo hilo. Biblia ilisema hivyo, "Maandiko si ya kufasiriwa apendavyo mtu." Ni Mungu Mwenyewe akiyafasiri. Angalia, Wengi hawakuona jambo hilo kwa sababu hawakuwa wameyachunguza Maandiko. Hawakuwa wamesikiliza yale aliyosema.

28 Wengi, siku hizi, hawajasikiliza Ujumbe, hawajasikiliza Maandiko na yale Kristo aliyoahidi katika siku hizi za mwisho. Hiyo ndiyo sababu watu wako kwenye hali waliyomo leo, na makanisa yameshikana moja kwa lingine. Hawajaona kile Maandiko yalisema kwa ajili ya siku hii. Hawakuona mambo haya yalipaswa kufanywa. Ni kutimizwa tu kwa Maandiko. Watu wengi wanampenda Yeye. Watu wengi wanamwamini. Lakini hata hivyo ni jambo la ajabu sana, hawawezi kulifahamu, unaposema habari Zake, kuwa Yeye yuko tu kama vile alivyokuwa jana, akifanya mambo yale yale. Wanadai wanaamini jambo hilo, lakini, linapotukia, basi hawalifahamu. Wao, hawawezi kamwe kuliamini.

29 Angalia, walikuwa wakizungumza habari Zake wakati alipotokea. Sasa, hilo ni jambo zuri. Tunaona hapa katika Maandiko, yalisema, "Na walipokuwa wakizungumza habari Zake, walipokuwa wakizungumza juu ya mambo haya, wakienda zao, wakisema habari Zake, wamehuzunika," ndipo walikuta kwamba Yeye alitokea. Na alipotokea, aliwatokea wakati walipokuwa wakienda zao, wakibadilishana mawazo juu Yake. Hapo ndipo Yeye anapotokea daima, ni wakati tunapozungumza habari Zake. Daima, kote katika Maandiko, ni wakati watu wanaponena habari za Mungu, hapo ndipo Yeye alipotokea.

30 Sasa sisi tunashughulikia sana kuzungumza juu ya mambo mengine. Nafikiri hiyo ndiyo sababu watu wengi, wanaompenda, hushindwa kumwona. Tunashughulika sana na kanuni zetu za imani na madhehebu, na shughuli za makanisa, na uanachama, na kuwapata wafuasi wengi na kadhalika, tunashughulika sana hata hatuwezi kuzungumza habari Zake. Yeye ni Neno. Tunavutiwa sana na yale... kanuni fulani za imani, kitabu fulani cha kiada, ama vile kitu kingine kinavyosema. "Tunaweza kuwaingiza wafuasi wangapi,

kuwapigia kura? Je! tumchukue *huyu*, *yule*, huyo mwingine?" Inatupasa daima kujitolea kwa Neno la Mungu na kwa maombi, tukilisoma Neno. Lakini tunavutiwa mno na kitu kingine.

31 Watu hawa walikuwa na huzuni. Walikuwa wakizungumza; jambo kubwa lilikuwa limetendeka; Yeye alikuwa ameondolewa. Bali walikuwa wakizungumza habari Zake, Naye huyo hapo akatokea. Na hapo alipotokea, Yeye alikuwa ni mgeni kwao. Hawakufahamu jambo hilo. Kwanza, Yeye alininii . . . kwanza, tunaona ya kwamba alikuwa akitembe- . . .

32 Walipokuwa wakienda zao barabarani wakielekea kwenye mji huo mdogo, Emau, maili chache tu ama mbili huko chini, mwendo wa Sabato, au kitu fulani; kwanza, Yeye alifunua Maandiko yaliyoahidiwa juu Yake, kwao, kwa ajili ya siku hiyo. Sasa angalia wakati Yesu anapojitokeza jukwaani, kama tukitaka kumwona na kuzungumza Naye baada ya kufufuka Kwake, kama walivyofanya, kama walivyomwona, jambo la kwanza alilowafanyia lilikuwa ni kujifunua kwao, kwa Maandiko. Amina. Hiyo ni kuyafanya nini? Wao walikuwa Waebrania. Waliamini Neno. Nao . . . Yeye, Yeye alijifunua Mwenyewe, alifunua Neno lililoandikwa juu Yake, yale aliyopaswa kufanya kwa wakati huo. Amina. Kila . . .

33 Mungu, katika Mwanzo, na halafu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yeye aliligawa, kisha akalinena na kusema yale yangetukia, tangu mwanzo—mwanzo hadi mwisho.

34 Siku zote makanisa hulishakia, nayo yanatoka, na mtu inambidi kuingiza yale wanayoamini juu ya jambo Hilo. Ndipo *huyu* anasema, "Vema, ninaamini tofauti kidogo na jambo hilo," naye anajifanyia kitu fulani. Naye huyu inampasa kufanya jambo fulani. Kila mmoja ana mnara, jiji, ama kitu fulani kinachowapasa kujenga, daima wakijaribu kuongeza kitu fulani ama kufanya jambo fulani, na kusema ya kwamba, "Tulifanya jambo *hili*." Loo, hivyo ndivyo unavyochanganyikiwa.

35 Ondoka kwenye picha. Acha Mungu alifanye. Unaona? *Hili* hapa Neno Lake, yale aliyosema angefanya. Kila wakati, Yeye humtuma nabii huko, akiwa ametiwa mafuta. Neno la Mungu humjia nabii, daima, kulithibitisha katika wakati huo.

36 Yohana Mbatizaji alijitokeza jukwaani. Yeye alikuwa ndiye nabii wa wakati huo. Alikuwa ndiye Nuru ya wakati huo, maana nabii, Malaki, alikuwa amesema habari za kuja kwake, "Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu." Isaya, miaka mia saba na kumi na mbili huko nyuma, kasema, "Sauti ya mtu italia nyikani, tazama na . . . " vile angefanya katika siku za mwisho, "kuyanyosha mapito nyikani," na mambo haya yote yaliyotabiriwa juu yake. Wakati alipojitokeza jukwaani, yeye alikuwa ndiye nabii wa kudhihirisha ahadi hiyo.

37 Yesu ndiye Neno, nalo Neno daima humjia nabii. Na kumbukeni, wakati nabii huyu alipokuwa akitabiri,

"akiyanyosha mapito," halafu wakati Neno alipokuwa duniani, Neno alitembea moja kwa moja akaingia majini na kumjia nabii. Amina! Ni kamilifu jinsi gani! Neno humjia nabii. Naye alikuwa Neno. Kwa kuwa, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu. Na—naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu, nasi tulimwona." Si ajabu Yeye alisema, "Inatupasa kwamba tutimize haki yote." Neno lilimjia nabii, majini, kutimiza haki yote.

38 Na tunaona basi ya kwamba alijifunua Mwenyewe kwa Kleopa na rafiki yake hapa. Huyo mwingine, hajulikani, kwa jina. Lakini ilikuwa Kleopa, tunajua, Naye akajifunua kwao, kwa Maandiko. Angalia vile Yeye—Yeye alivyosema.

39 Angalia, wao, wao walimwita "Nabii." "Hamjui mambo haya? Yesu wa Nazareti, Nabii ambaye Mungu alijidhihirisha Kwake." Mnaona? Ambaye, mbele za watu wote, na kadhalika, Yeye aliitwa Nabii. Basi kama walikuwa wamemtambua Yule waliyekuwa wakizungumza habari Zake, kuhusu kuwa Nabii, inaonekana kana kwamba wangaliona papa hapa ya kwamba Nabii yuyo huyo alilichukua Neno tena na akaanza kulifunua.

40 Ambalo, Yeye alikuwa ndiye hilo Neno, Naye alikuwa akijifunua, kwa mdomo, Neno lililoandikwa juu Yake. Naye akaanza, na Yeye akaanzia kwa Musa, na kuwaelezea yote ambayo manabii walikuwa wamesema kumhusu Yeye. Loo, jamani! Jinsi alivyolitambulisha kwa ajili ya wakati huo! "Enyi msiofahamu, wenye moyo mzito. Tukijua ya kwamba Musa na manabii wote walisema ya kwamba Kristo hana budi kuteswa na kuingia katika Utukufu Wake." Unaona, na kwa ajili ya wakati huo, hayo ndiyo yaliyopaswa kutukia. "Je! Hamjui ya kwamba Yeye anapaswa kufanya jambo hilo?" Unaona, akifunua Neno lililoandikwa juu Yake.

41 Hivyo ndivyo Kristo anavyofanya daima. Mungu kamwe habadilishi mpango Wake. Jinsi anavyolifanya mara ya kwanza, ndivyo anavyofanya kila wakati. Yeye alifanya uamuzi, katika Bustani la Edeni, wakati mwanadamu alipopotea, kumwokoa kwa Damu iliyomwagika. Hapo ndipo mahali pekee angewahi kamwe kukutana na mwanadamu. Hapo ndipo mahali pekee amewahi kukutana na mwanadamu, tangu wakati huo. Ni chini ya Damu iliyomwagika.

42 Tumejaribu kuwaelimisha. Tumejenga minara. Tumejenga miji. Tumejenga chochote kingine, tukijaribu kuwaunganisha watu. Tumejaribu kuchukua elimu na kuwaunganisha pamoja. Tumejaribu kuchukua nguvu za kijeshi na kuwaunganisha pamoja. Tumejaribu madhehebu, kuwaunganisha pamoja. Yote yameshindwa.

43 Mungu ana mahali pamoja, hapo ni chini ya Damu. Hiyo ndiyo njia pekee. Chini ya Damu, Yeye atakutana na mwanadamu. Nao ni ndugu waliozaliwa kwa Damu.

44 Natumaini siwapigii makelele sana huko nje, kwa hiki, lakini inasikika kana kwamba kuna kurudishwa mwangwi. Kama ndivyo . . . Je! mnaweza kunisikia vizuri? Kama mnaweza, inueni mikono yenu. Vema. Sasa, ili tu nijue ya kwamba mnalipata Hili; hamna budi kulipata.

45 Angalia sasa, wakati Yeye aliposema, wangali walishindwa kumtambua kwa Neno lililoandikwa. Wazia jambo hilo! Wakati alipokuja na kujifunua Mwenyewe kwa Neno, kwao, nao bado walishindwa kuliona.

46 Kama hiyo siyo picha ya siku hizi, sijui ni kitu gani. Wangali wanashindwa, wakati Maandiko yanasema mambo haya. "Itakuwa katika siku za mwisho," asema Mungu, "Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu na binti zenu watatoa unabii. Juu ya wajakazi Wangu na watumishi wanawake nitaimwaga Roho Yangu, katika siku hiyo. Nitaonyesha maajabu juu mbinguni, na moto na moshi, na kadhalika." Wangali hawalioni.

47 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu; watakuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa. Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Mambo hayo yote ambayo wamesema habari zake, na Neno lililohubiriwa kutoka jukwaani, na hata hivyo wengi wanaompenda hawalioni. Wangali wanapapasa gizani. Wangali wanashindwa kumjua Yeye, kwa Neno lililoandikwa.

48 Wanachukua seminari, nao wanapotoka na kulifasiri vibaya, na kila kitu, na kulirudisha, wala kamwe hawajui wa—waamini kitu gani duniani. Mmoja anasema liko *hivi*, na mmoja anasema Liko *vile*. Basi ni Neno lililoandikwa tu, Yesu kamwe hakuwaambia waende ulimwenguni kote na "kufundisha." Yeye alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili." Tofauti kubwa sana, kujaribu kufundisha jambo fulani, na kuhubiri jambo fulani. *Kuhubiri* ni "kudhihirisha." Itabidi lifanye hivyo, kuonyesha nguvu za Roho Mtakatifu. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Inahitaji Roho Mtakatifu kudhihirisha Neno hilo. Kama ni Kweli, Neno, Mungu atalidhihirisha. Kama si Kweli, Mungu hatakuwa na uhusiano wowote nalo, maana Mungu hatajizongomeza Mwenyewe na uongo, mnajua jambo hilo, kwa sababu Yeye ni Mungu sasa, vivyo hivyo sasa.

49 Walidai ya kwamba walikuwa wameamini, nao walikuwa ni wanafunzi Wake, walimpenda, waliamini jambo hilo, Naye alikuwa amesimama moja kwa moja pamoja nao, akilifasiri Neno, kwamba Yeye alikuwa ni Nani, na hata hivyo wao hawakujua hilo. Wazia tu jambo hilo! Hawakujua hilo, Naye akisimama pale Mwenyewe, yameandikwa katika Maandiko,

na anarudi nyuma na kuyachukua Maandiko, yaliyokuwa yameandikwa miaka mia kadhaa, kumhusu Yeye, na akisema jinsi ambavyo hana budi kufanya na mambo haya yote namna hiyo, nao wanatembea kote na kusema, "Usiniambie? Vema, unajua nini!" Naye, Yeye akizungumza, nao wangali hawakutambua jambo hilo.

50 Ni picha ya jinsi gani ya siku hii! Vile vile na sasa, wanadai wanaamini ya kwamba Yeye alikuwa amefufuka katika wafu, bali, wakati anapotokea kujionyesha Mwenyewe, wangali hawaamini hilo. Unaona? Hata hivyo, wanadai wanaliamini. "Loo, naam, tunaamini Yeye alifufuka siku ya tatu." Hebu afanye jambo fulani kuonyesha ya kwamba alifufuka siku ya tatu; "Loo, siamini jambo hilo." Unaona? Haya basi, jambo lile lile.

51 Angalia, Yeye alisema, "Enyi msiofahamu, na wenye moyo mzito kufahamu ahadi ya Maandiko kwa ajili ya wakati huu."

52 Wasiofahamu walisema, "Loo, Yeye ameondoka. Walimsulubisha, nasi tulifahamu ya kwamba Yeye alifufuka tena, lakini, loo, jamani, hiyo ni hadithi tu ya fumbo ambayo mtu fulani alihadithia. Hatukujua lolote juu yake. Loo, ninawaambia, ni jambo la huzuni mno!"

53 Akasema, "Enyi msiofahamu, na wenye mioyo migumu kufahamu yale Maandiko yaliyosema kwa ajili ya wakati huu." Amina.

54 Haya basi. Laiti ningaliweza kulilipua hilo kwenye Baraza la Ekumeni. Naam, bwana. Wenye mioyo mizito, mkijua Maandiko yanasema mambo haya; mngali hamfahamu jambo hilo. Haya basi.

55 Akasema, "Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito kufahamu Maandiko yaliyotabiriwa kwa ajili ya siku hiyo, na jinsi hasa ambavyo lingetukia, na hili hapa limetukia. Kristo aliingia katika Utukufu Wake, kwa kuteswa kwanza, akiwa amekufa; na akafa, akafufuka tena siku ya tatu. Je! . . . Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema Yeye alipaswa kufanya, kufufuka katika siku ya tatu." Akasema, "Hii ni siku ya tatu tangu lilipotukia."

56 Kasema, "Vema, hayo ndiyo ninayojaribu kuwaambia!" Na bado hawakufahamu jambo hilo. Ndipo akasema, "Ninyi hamfahamu, na mna mioyo mizito kufahamu yote ambayo manabii wamesema, na yale Maandiko yanayosema kuhusu siku hii. Na hapa imetendeka moja kwa moja mbele yenu, wala hamjui jambo hilo."

57 Wakasema, "Vema, unajua nini!" Unaona, macho yao yalikuwa mapofu.

Unasema, "Yaweza kuwa yamepofuka leo hii?" Naam, bwana.

58 Yamepofuka leo kama ilivyokuwa wakati huo. Kweli. Hivi Biblia haikusema, "Wangekuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapenda anasa zaidi kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiowapenda wa kwao; wenye mfano wa utauwa, bali wangekana Nguvu zake, Nguvu za ufufuo na kudhihirishwa kwa Mwana wa Mungu"? Biblia ilisema hilo lingetukia, kwa hiyo halina budi kutukia. Kama tu Yeye alivyosema, Isaya alinena na kusema, "Mna macho wala hamwezi kuona, na masikio wala hamwezi kusikia." Mungu yule yule alisema Maandiko yale yale.

59 Tunaona, basi, Paulo, ule ufunuo mkuu aliokuwa nao wa Yesu Kristo, kwamba Yeye alikuwa ni Nani, lilikuwa ni jambo kubwa sana kujua. Vema, Mungu aliuweka katika Biblia, hivyo ndivyo ulivyokuwa mkubwa. Hiyo ndiyo sababu alipewa mwiba mwilini, kumshusha chini kusudi asijiinue na kujikweza. Mungu alimshusha chini, na kumfanya mdogo, kusudi apate kumtumia katika sehemu mbali mbali za nchi, apate kumfanyia yale aliyotaka, kwa sababu yeye alikuwa na ufunuo wa Yesu Kristo, kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

60 Basi angalia, hili hapa jambo la kufanya. Jambo la pili tunalopata, walimkaribisha aingie ndani. Akafika mahali hapo padogo, mkahawa mdogo ambamo walikuwa watakaa. Kulikuwa kunaelekea kuchwa, nao wakasema, "Loo, njoo ukae pamoja nasi." Alifanya kama anataka kuendelea mbele.

61 Loo, niliwazia jambo hilo mara nyingi. Yeye anakutaka tu umwalike. Alifanya kana kwamba anataka kuwapita. Huenda akafanya kana kwamba atakupita, dada, uliye kwenye kiti cha magurudumu; ama wewe, bwana, kwenye machela; ama wewe, huko nje ukiwa na ugonjwa wa moyo, ambaye huwezi kuishi ila muda mfupi tu zaidi. Watu hawa labda wamelemaa, huenda wakaishi wakati wa kawaida wa maisha; bali mtu fulani huko nje mwenye ugonjwa wa moyo, huenda akafa kabla ya asubuhi, huenda akafa kabla ya kesho. Huenda Yeye akafanya kana kwamba anataka kukupita, bali Yeye anataka tu umwalike aingie. Unaona?

62 Huenda ukawazia, "Vema, Yeye alimponya *fulani*, hivi majuzi. Yeye, mwezi uliopita, ninajua, miaka miwili iliyopita, niliona. . . " Naam, huenda akafanya kana kwamba atakupita, bali anataka tu u—umwalike. Anafanya kana kwamba atapita. Kile alichokuwa wakati huo, ndicho alicho leo. Anachofanya wakati huo, anakifanya leo. Alisema hivyo. Angalia, huna budi kufanya jambo lilo hilo, huna budi kumwalika aingie ndani. Ilikuwa ni wakati huo, na wakati huo pekee, ambapo Yeye angeweza kujifunua Mwenyewe.

63 Asingefanya hivyo kwa kuwahubiria Neno. Lilipita juu ya kichwa chao. Yeye akitembea pale, akisema, "Vema, mlipaswa kujua pale, enyi msiofahamu, wenye moyo mzito. Biblia

ilisema mambo haya, ya kwamba Kristo hana budi kufanya mambo haya, na kadhalika." Akitembea pale, vema, inaonekana kana kwamba wangeweza kuona Huyo alikuwa Ndiye. Yeye hakutokea wazi wazi na kuwaambia, "Mimi ndiye." Ukimpata jamaa anayefanya hivyo, basi utajua yeye hana lolote, kwanza. Lakini alimwacha tu Roho Mtakatifu afunue jambo hilo. Alitwambia.

64 Yeye alimwambia yule Farisayo, kasema, "Yachunguze Maandiko, ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yanawaambia kwamba Mimi ni Nani." Wanapaswa kujua jambo hilo. Vivyo hivyo wanapswa kujua, leo, si chungu nzima ya ghasia, ama kuzozana, ama tendo la kijinga, ama kelele nyingi. Ni Yesu Kristo akidhihirishwa miongoni mwa watu Wake. Naam. maandiko yanasema hivyo. Angalia, sasa, na hilo linalifanya kweli wakati Mungu anaposema hivyo.

65 Tunaona sasa, jinsi tu anavyoweza kufunua ni kuingia ndani yako. Yeye ni, Yeye anaweza, Yeye ni Neno. Nalo Neno, ndani yako, ndipo Roho Mtakatifu anamfunua Kristo, kupitia Neno, baada ya Yeye kuingia ndani yako. Yeye yumo ndani yako. Huna budi kulichukua Neno Lake.

Unasema, "Vema, kanisa langu haliamini jambo Hilo."

66 Vema, kamwe hutaweza kuingia. Unaona? Unapolikataa Neno, unamkataa Yeye.

"Vema, kanisa langu linaamini kulifanya Hivi."

67 Lakini Biblia inasema lifanye namna *hii*. *Hii* ndiyo njia. Lichukue kama lilivyoandikwa Mle. Si kile mtu mwingine ameongezea Kwalo, bali yale Mungu aliyosema kulihusu. Na ndipo Yeye angeweza kukufunulia, bali inabidi Yeye kuingia ndani yako, kwanza. Ndipo, na ndipo tu, anapoweza kulifunua.

68 Usisimame na kujaribu kuliangalia na kujaribu kulielewa, kama vile yule Farisayo alivyosema. Walisimama na kumwangalia pale, kasema, "Mtu huyu ni Beelizebuli." Wasingeweza kulielewa. Iliwabidi kulipa jina. Wao walisema, "Mtu huyu hufanya hivi kwa roho wa ibilisi. Yeye, Yeye ni Beelizebuli, mpiga ramli. Mbona, msiwe na uhusiano wowote na Mtu huyu. Yeye alizaliwa katika dhambi. Hana kadi zetu za ushirika. Yeye si wetu. Na, loo, jamani, wao . . . Hata hatujui alikoenda shuleni. Hana elimu. Mbona, vema, Mtu huyu alitoka wapi? Sasa Yeye anasema, 'Ati Mwana wa Adamu atakayepaa juu, aliyeshuka chini'? Yeye alizaliwa papa hapa. Ana kichaa. 'Ati msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, muinywe Damu Yake'? Yeye ni mla watu." Naye alifanya hivyo kusudi tu awafanye waseme mambo hayo. Iliwabidi kufanya hivyo.

69 Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu, leo, akilionyesha Neno Lake, katika dhihirisho, kusudi watu walihukumu, ili Mungu apate kuweka hukumu Yake juu ya nchi, kama alivyoahidi atafanya.

Yeye aliufanya mgumu moyo wa Farao. Haleluya! Ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Habadiliki. Yeye ni Mungu. Mifumo Yake ya kufanya mambo, anajionyesha Mwenyewe mwenye nguvu kwa Neno Lake, kulidhihirisha. Haimbidi kukwambia mambo yote kulihusu. Haikubidi kulielewa. Huwezi kumwelewa Mungu. Inakubidi kulikubali. Mwalike tu aingie ndani uone kile kitakachotendeka.

70 Sasa, tunaona tena jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe kwao, akisha kuingia. Alifanyaje jambo hilo? Aliyafungua macho yao kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Alipoingia ndani yao, ndipo aliyafungua macho yao, wapate kuona.

71 Sasa wakati Neno linapoingia ndani yako, unapolikubali Neno la Mungu nalo linaingia ndani yako, basi ahadi (ya hiyo ahadi ambayo umeikubali) hujidhihirisha, ndipo unajua kwamba ni Nani.

72 Alifanya hivyo kwa njia gani, alijitambulisha namna gani kwao? Kwa sababu alifanya mambo yale yale aliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake. Ndipo wakajua ya kwamba huyo alikuwa Ndiye, kwa maana alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Mahubiri yote, mafundisho yote, na yote yale aliyokuwa amefanya, yalikuwa yameshindwa. Lakini wakati alipojifunua Mwenyewe, akifanya jambo lile lile alilofanya kabla ya kusulubishwa Kwake, walijua ilikuwa ni Yeye. Lilifungua macho yao.

73 Ndugu, dada, ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Habadiliki. Kama tu alivyomfanyia yule mwanamke pale kisimani, unaona, kamwe Yeye habadilishi mpango Wake.

74 Sasa, maskini mwanamke huyu pale kisimani, alijua ahadi ya Maandiko kwa ajili ya siku hiyo. Angalia wakati alipomjia maskini mwanamke yule kisimani. Yeye alisema, huko Sikari, alisema, "Ewe mwanamke, nipe maji ninywe."

75 Akasema, "Mbona, si kawaida kwenu Wayahudi kutuomba sisi Wasamaria kitu kama hicho."

76 Akasema, "Lakini ungalijua ni Nani unayesema naye, ungaliniomba Mimi maji."

77 Vema, ndipo akawazia, "Kimbelembele fulani huyu, kwa hiyo nitampiga swali tu kidogo." Akasema, akaanza kumhoji.

Mara akasema, "Nenda kamwite mumeo uje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

78 Kasema, "Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa siye mume wako."

79 Angalia! Upesi, lilifanya nini? Liliingia ndani. Upesi, yeye alijua jambo fulani. Kasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii." Amina. Unaona, kulikuwako na mbegu iliyokuwa pale, ipate kuwa Hai. Kulikuwako na swichi pale ambayo ingewasha

Taa. Kwao Mafarisayo, ilikuwa ni giza, kwa kuanzia; hamna swichi, hamna betri, hamna kitu chochote kile. Lakini kwa Mtu huyu; mwanamke huyu, maskini kahaba, alisema, "Bwana!"

80 Kwa nini? Alikuwa akitarajia dhihirisho la Neno. Miaka mia nne tangu Malaki, hawakuwa na manabii, na huyu hapa Mtu aliyedhihirika kuwa nabii. Upesi alijua hicho kilikuwa ni kitu fulani. Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii." Akasema, "Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, hayo ndiyo atakayokuwa akifanya."

81 Akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye." Sasa Yeye anaweza kujifunua Mwenyewe. Yeye amekwisha kumpokea tayari. Yuko ndani sasa, unaona, anaweza kujitambulisha. Hivyo ndivyo Yeye alivyojitambulisha kwa ulimwengu, mwanamke. Kwa nini? Yeye aliamini Neno lililoahidiwa, na wakati alipoona Neno lililoahidiwa likidhihirishwa.

82 Sasa tunajua, katika Kumbukumbu la Torati mlango wa 18, kifungu cha 15, Musa alisema, "Bwana Mungu wako atakuondokeshea nabii kama nilivyo mimi." Naye alijua ya kwamba Masihi huyo atakuwa nabii. Na nabii wa mwisho alikuwa amekoma, miaka mingi, mingi sana kabla ya hapo. Hakukuwako na manabii wowote. Na hapa alisimama Mmoja. Ilikuwa ni kitu gani? Lilikuwa ni jambo lililofuata. Hilo lilikuwa ni Neno. Alifanya nini? Alilifunua kwake, kwa kumwambia, kufunua ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye nabii yule, kwa kufunua yale aliyokuwa amefanya. Loo, jamani!

83 Hilo lilitosha. Aliacha mtungi huo wa maji, akakimbia kwenda mjini, na kusema, "Njoni, mumwone Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Ati kumzuia? Mbona, usingeweza kufanya jambo hilo; ilikuwa ni kama kujaribu kuzima moto kwenye siku yenye upepo, na nyumba iliyokauka ikiungua moto. Naam, bwana, ilikuwa ikiungua na kuwaka moto kwa nguvu. Mungu alikuwa ametenda jambo fulani. Alikuwa ameona jambo fulani. Alijua lilikuwa ni Kweli. Neno lilikuwa limedhihirishwa mbele zake. Kama tu vile hasa ilivyokuwa kwa wanafunzi baadaye, unaona, wakati Yeye alipokuwa akijaribu kuwaonyesha Neno, na halafu akalidhihirisha Neno hilo. Naye hapa alilijua hilo Neno, na, wakati alipoliona likidhihirishwa, hilo lilitosha.

84 Siku moja, mtu mmoja jina lake Andrea aliyekuwa akimwangalia Yohana, akimsikiliza akizungumza juu ya Masihi ajaye. Petro alikuwa ni ndugu yake; hakuvutiwa. Walikuwa na baba mzee mcha Mungu aliyekuwa amewafundisha, "Sasa, mwanangu, tumemtumainia Mungu kwa kila kitu tunachohitaji. Siku ambazo madeni yetu yasingeweza kulipwa, tuliomba, 'Mungu, tupe samaki wengi leo.' Tungetoka tukaenda, na Mungu angetupa hao samaki wengi. Na tulipowavua hao samaki, tungefanya nini? Tungeingia na kumsifu Mungu kwa ajili ya

jambo hilo, na kuwauza samaki wetu. Tumemtumainia Mungu. Mimi ni mzee sasa. Labda sitakuona kuja kwa Masihi. Lakini, angalieni. Kabla hajaja, kutakuwa na madhihirisho mengi ya uongo."

85 Na Biblia ilisema yalikuwako. "Makristo wa uongo waliinuka." Hiyo ni kweli. Ilikuwa ikifanya nini? Kujaribu kuzima taa ya Yule wa kweli ajaye. Mnaona? Tumekuwa na madhehebu mengi, makundi mengi, na kila kitu chochote kilichoinuka, na kuwapeleka Canada na kuwaingiza kwenye maficho mahali fulani, huko juu mahali pengine, na kuongoza kundi moja upande *huu* na upande *ule*, ikijirudia tu vile vile tena. Inajaribu kufanya nini? Inajaribu kufanya nini? Yeye anajaribu kuzima Taa ya Kweli. Sasa tunaona.

86 Ndipo siku moja, Petro alikuja ufukoni, kuvua samaki, na kuosha nyavu zake. Ndipo Yesu akashuka akaja. Na jambo la kwanza twajua, kwamba, mara alipojitokeza mahali alipokuwa Petro . . .

87 Yeye alikuwa amefunzwa vizuri, yale Masihi huyo angefanya. Baba yake mzee alimwambia, kasema, "Sasa Simoni, Maandiko yanasema. Wewe ni, unakumbuka, wewe ni Myahudi. Bwana ametwambia, 'Akitokea mmoja kati yetu, ambaye ni wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitasema naye.' Na kama Yeye, yale anayosema ni Kweli, Kweli iliyodhihirishwa, na yale asemayo yanatimia daima, basi mnajua Yeye ana ufunuo wa Kiungu wa Maandiko. Sasa mtamtambua Masihi wakati mtakapomwona."

88 Kwa hiyo alienda moja kwa moja mbele za Yesu, siku moja. Akawazia, "Nitaenda nikaone yale Andrea aliyokuwa akisema habari zake."

89 Na mara alipofika Kwake; Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hilo lilitosha. Hilo lilitosha, kwa kuwa alifundishwa mle ndani ya kwamba Yeye angekuwa ni nabii. Alijua jambo hilo.

90 Kulikuwako na maskini mwanachuoni mwingine aliyekuwa akifundisha; wakati Filipo alipokuwa amesimama pale akiangalia mambo hayo yakiendelea. Alikimbia kuuzunguka mlima, upesi sana, basi akampata mtu mwingine, jina lake Nathanaeli, ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa Biblia, msomaji. Walikuwa wameyasoma Maandiko, maana walijua wakati ulikuwa umekaribia. Walikuwa wakimtarajia aje.

91 Hao ndio Yeye anaowajia, kwa wale wanaomtazamia. Nasi tunaona, leo, Yeye haji kwa wale wasiomtazamia. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu kwa—kwa wale wasiouamini. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa hao wasiouamini. Ni kwa wale tu wanaouamini. Hiyo ni kweli. Hivyo tu. Kwa hiyo basi tunaona, wale wanaotarajia kujua Kweli, Mungu anawajibika kuwafunulia ile Kweli. Yeye hutamka Neno Lake, kisha anakuja na kulitimiza, kutoa tafsiri Yake Mwenyewe.

92 Sasa tunaona, mara maskini mwanamke yule, yeye alisema...Asingeweza kuelewa jinsi Mtu huyu alivyokuwa akijifanya mwerevu kwake, akasema, kuhusu kumpa maji anywe, na akasema, ama kumpa Yeye maji anywe, na kujaribu kujifanya mjuaji. Na muda si muda mwajua, mbona, alianza kuzungumza Naye, na, akaja kutambua, akasema, "Tunajua yuaja Masihi, na, ajapo, atatwambia mambo haya."

93 Akasema, "Mimi Ndiye, ninayesema nawe." Ndipo macho yake yakafunguka. Macho yake yakafunguka. Na nini? Ahadi ya Maandiko. Macho yake yalifunguliwa na ahadi ya Maandiko.

94 Petro alijua ya kwamba baba yake alimwambia ya kwamba Masihi huyo angekuwa nabii. Na hapa Yohana alikuwa amemwambia, ama Andrea alikuwa amemwambia juu ya nabii, Yohana, alikuwa mahali fulani huko akitabiri, na kadhalika, akisema jambo fulani lingetukia. Kwa hiyo siku moja alishuka akaenda kule, baada ya Yesu kuja. Alipofika Mbele Zake, alisema, "Wewe ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona." Ilikuwa ni kitu gani? Macho yake yalifunguliwa. Alijua jambo hilo.

95 Filipo na—na Nathanaeli walikuwa wakisoma Maandiko kuhusu kuja Kwake. Akaja, akasema, "Njoo, umwone Yule niliyekutana naye, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

"Loo," akasema, "hakuna lolote jema linaloweza kutoka Nazareti."

Kasema, "Wewe njoo, uone."

96 Nao haoo wakazunguka mlima. Hapana shaka walisimuliana juu ya mambo mengi ambayo Yesu alikuwa akifanya, yale aliyokuwa amemwambia Simoni, yale aliyokuwa amefanya, mambo haya aliyokuwa amefanya.

97 Mara Filipo alipoenda Mbele Zake, pamoja na Nathanaeli, Yesu alimwangalia Nathanaeli, na kusema, "Tazama Mwisraeli ambaye ndani yake hamna hila."

Akasema, "Rabi, ulinitambua lini?"

98 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona." Macho yake yakafunguka.

99 Akasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli." Ilikuwa ni kitu gani? Aliona Neno lililoahidiwa la siku hiyo limefunuliwa.

100 Sikiliza, ndugu, dada, Neno lililoahidiwa lingeweza kuahidiwa kwako, nawe unaweza kuona ni wakati wa hilo; bali Mungu anapolifunua, anapolifasiri, basi ni dhambi kulipuuza. Kamwe usifanye hivyo. Mungu aliyafungua macho yake, kwa kumwonyesha Neno lililodhihirishwa ambalo Yeye alikuwa ameahidi kwamba lingetukia. Sasa, daima Yeye hufanya jambo hilo jinsi anavyolifanya, kamwe Yeye habadilishi mfumo Wake katika kufanya jambo hilo. La. Kwa hiyo, kumbukeni, ni vivyo hivyo daima. Yeye aliahidi Maandiko kwa kila wakati, na,

wakati anapodhihirisha Maandiko hayo yaliyoahidiwa kwa ajili ya wakati huo, watu wanaofunguliwa macho yao kuliona ndio wanaolipokea.

101 "Sasa, Ndugu Branham," unasema, "kunachelewa, basi utasema nini sasa."

102 Ahadi ya Kimaandiko ya wakati huu ni ipi, tupate kujua tunachonena habari zake? Tupo hapa kwa sababu gani usiku wa leo? Ina faida gani? Je! tunaishi karibu na kitu fulani? Je! kweli tunaamini? Je! tumeshuhudia bure? Je! tunasema tunaamini Yeye anakuja? Je! tunaamini Uwepo Wake unaoonekana? Je! tunaamini ya kwamba Yeye anakuja mara ya Pili? Ama, tunajifanya tu kupumbazwa, ama kweli tunaamini?

103 Hebu na tuyachunguze Maandiko basi na tuone ni kitu gani kilichoahidiwa kwa ajili ya siku hii, ndipo tuseme, kama yule mwanamke kisimani, Filipo na hao wengine, "Tunaweza kuona."

104 Kumbukeni, Waebrania 13:8 ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye aliahidi jambo hilo. Hayo ni Maandiko.

105 Yohana Mtakatifu 14:12 ilisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Ninawekea jambo fulani msingi.

106 Sasa katika Yoeli 2:28, na 2:28 na 30, na kuendelea, Yeye aliahidi. Alisema, "Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu; na yaliyosazwa na madumadu, yameliwa na *ninii*." Kila mmoja wa hao wadudu ni mdudu yule yule; anabadilisha tabia yake. Madumadu ni tunutu, na kadhalika. Ni katika hatua mbalimbali za safari yake, na anakula tu na kula na kula, na alikula mti huo wa Mungu moja kwa moja mpaka kwenye shina. Basi kweli mti huo utaishi tena? Lakini, ulionekana hauna matumaini, bali Mungu alisema, "Nitawarudishia," asema Bwana, "miaka yote iliyoliwa na madumadu, tunutu. Walichokula, nitakirudisha katika nguvu zake tena."

107 Yaliyosazwa na Walutheri, yameliwa na Wamethodisti; yaliyosazwa na Wamethodisti, yameliwa na Wapentekoste; yaliyosazwa na Wapentekoste, yameliwa na akina *nanii*; kuendelea tu chini, chini, chini; mmoja likiwa na *hili*, na mmoja na *hili*, na mmoja na *hili*, na mmoja na *hili*, na mmoja na *hili*, mpaka lote likafifia likawa ni kundi la itikadi nyingi. Tunajua hiyo ni kweli. Ninasimama kati yenu, na ninawapenda.

108 Lakini, kumbukeni, katika Malaki 4, sio Malaki 3 sasa, Malaki 4, Mungu aliahidi kutuma upako tena na "kuirudisha Imani ya watoto iwaelekee baba zao tena." Na ni vile hasa Mungu alivyoahidi, Yoeli. Litatendwaje? Tunaona ya kwamba Yesu alisema, katika Luka 17:26 hadi 30, Yeye alisema jambo hilo katika ninii wa 27. . . Luka 17, Yeye alisema, "Kama

ilivyokuwa katika siku za Nuhu, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa; wala hawakujua mpaka Nuhu alipoingia ndani. Ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Lakini Yeye alisema, pia, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu."

109 Je! mliwahi kurudi nyuma? Laiti tungalikuwa na wakati wa kurudi nyuma na kulifunua tu hilo. Kurejea katika Mwanzo, hicho ni kitabu kile kile ambacho Yesu alikuwa akisoma. Hicho ndicho alichokuwa akifunue, alichokuwa akisema habari zake. Rudini kule nyuma, angalieni hili alilosema. Na wana wa wanadamu... "Wana wa Mungu walijitwalia binti za wanadamu." Wanawake, tafsiri ya asili ya Kiebrania pale inasema walikuwa ni wanawake. "Waliwatwaa wanawake," unaona, "walijitwalia."

110 Angalia tu siku hizi, angalia kuoa, na kuolewa, "wala hawakujua mpaka."

111 Angalia hapa, angalia Uingereza, fedheha hii kuu, angalia hapa Marekani, angalia ukahaba, angalia kila kitu. Ni kama tu vile yule mchekeshaji alivyosema hivi majuzi usiku, ya kwamba, "Wanawake wanavaa mavazi yanayowabana sana, ni wazinzi sana wanapotembea barabarani; jambo lifuatalo watakalofanya ni kazi ya kujinyunyizia tu rangi, haitawabidi kutumia nguo." Karibu ni kweli kabisa. Waangalie jinsi wanavyoenda huku na huko, jinsi walivyo watovu wa uadilifu na wachafu na walivyo kinyaa, wanavyotembea. Na ukichukua, ukitoa mzaha, na kuketi kati ya wanaume, na kitu kama hicho, na kusema, "Jinsi tu unavyoweza kuwatambua...Wanavaa kama mwanamume, nao wanaume wanavaa kama mwanamke. Ni vigumu...wanakata nywele zao vile vile, vile vile. Jinsi tu unavyoweza kuwatofautisha mmoja na mwingine; kama ukitoa mzaha mchafu, mwanamume ataona haya, mwanamke hataona." Naam.

112 "Na binti wa Zayuni wangetembea kwa hatua za madaha katika siku za mwisho." Watashindwa kumfuata Bwana. Haidhuru utawaambia nini, unaweza tu kuhubiri na kuhubiri na kuhubiri, ni kama tu kupiga ukuta ule *pale*. Ni giza nene mno juu yao. Hakuna...inaonekana ni vigumu sana kumpata mwanamume halisi ambaye ni mwanamume, na kumpata mwanamke ambaye kweli ni wa heshima.

113 Angalia mitaani siku hizi, na kwenye skrini zetu, na popote pale, vipindi hivi visivyokaguliwa, kuvuta sigara, ukaidi, kufanya yasiyofaa, kuvaa kama mwanamume, na kadhalika. Yesu alisema mambo hayo yatakuwako, nayo yapo hapa. Hayahitaji kufunuliwa kokote; tayari yamefunuliwa.

114 Sasa angalia, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu," angalia hali ya mambo katika siku za Lutu, Mungu alishuka. Ndipo watu wawili wakashuka kwenda Sodoma na

kuhubiri huko Sodoma. Mtu Mmoja aliketi kule juu pamoja na Ibrahimu, Kanisa Teule, mfano wa mpentekoste aliyeitwa atoke siku hizi, asiye huko nje Sodoma.

115 Wale wanaoishi miongoni mwa Wapentekoste, na wanawake wanaokata nywele zao, na wanaume wanaofanya mambo kama hayo, na kufanya hiyo mizaha michafu, na kufanya yasiyofaa, hao si Wapentekoste, wamejibandika tu jina la kipentekoste. Wao si Wapentekoste. Mabibi halisi wa kipentekoste ni mabibi. Wanaume halisi wa kipentekoste ni wanaume.

116 Shule karibu zifungwe, kwa sababu ya vijana wanaume waliopotoka kuwa wapotovu na vitu kama hivyo, katika shule hizo, walawiti kote kote kila mahali. Ni tamasha tu la kuhuzunisha sana! "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

117 Kumbukeni, angalieni papo hapo, hicho kifungu cha 30, "Atakapofunuliwa Mwana wa Adamu." Ulipata kuona jambo hilo? Angalia hicho kifungu cha 30, "Atakapofunuliwa Mwana wa Adamu, katika siku kama ilivyokuwa kabla ya Sodoma." Angalia kilichotukia huko Sodoma. Mtu huyu alibaki nyuma. Wawili wao walishuka wakaenda huko chini, wakazungumza na—na Lutu, wapate kumtoa kule, wala ha—hakufanya miujiza yoyote kule chini, aliwapiga tu kwa upofu. Lakini huyu huku nje alifanya mwujiza, mbele ya Wateule. Alikuwa ameuelekeza mgongo Wake kwa Sara, naye alikuwa he—hemani nyuma Yake. Kasema, "Yu wapi Sara, mkeo?"

Kasema, "Yumo hemani, nyuma yako."

118 Kumbuka, Yeye alimwita "Sara," akamwita "Ibrahimu." Siku moja hapo kabla, yeye alikuwa Abramu; naye mke alikuwa Sarai, sio Sara.

Pia tazama, alisema, "Yumo hemani nyuma Yako."

119 Akasema, "Nitakuzuru." Ilikuwa kitu gani? Mungu katika mwili. "Nitakuzuru kulingana na ile ahadi."

Ndipo Sara akacheka, na kusema, "Mambo haya hayawezekani."

120 Akasema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema, 'Mambo haya hayawezekani'?" Akamwambia yale aliyokuwa akifanya. Yeye alikuwa ni Neno katika mwili wa mwanadamu, alijua siri za moyo wake, na kusema, "Kweli ulicheka!"

121 Na wakati alipofanyika mwili duniani, hivyo ndivyo alivyofanya hasa.

122 Naye alisema nini? "Wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Kama Walawiti wako kote nchini, ulimwengu wote umechafuliwa na umekwisha, na tunaona kanisa limekwisha, basi ni wakati ambao Mwana wa Adamu

anajifunua Mwenyewe: yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ndiyo ahadi ya Mungu.

123 Angalia yale aliyosema. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Mtaniona Mimi; mwaminio." Yeye yule jana, leo, na hata milele! Naam. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena." Hauwezi kumwona; macho yao ni mapofu.

124 Lakini mnapoona Mwana wa Adamu amefunuliwa, Neno limerudi katika mwili wa mwanadamu! Mtu aliyekula nyama ya ndama, akanywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, akala keki zilizookwa mekoni, naye aliitwa "Elohimu," amina, Mtu aliyevaa nguo zenye vumbi, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Huyo hapo duniani, amedhihirishwa katika mwili, na akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa katika siku za mwisho, dunia ingekuwa katika hali ya Sodoma," nayo ndiyo hii hapa. Ndugu, dada, mabibi na mabwana, vyovyote mlivyo, hii ndiyo saa hiyo, na fasiri ni ya Mungu. Mungu na ayafungue macho yetu yaliyopofuka kwa ahadi ya Kimaandiko, tujue ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Amina!

Na tuinamishe vichwa vyetu.

125 Baba wa Mbinguni, mengi sana yangeweza kusemwa. Hayo yanatosha. Nitasimama. Bwana Mungu, Wewe uliyefanya ahadi hiyo, jitokeze, Bwana, ifunue. Mwili wetu haufai kitu, mwili wetu ni mnyonge, na ni—ni mgonjwa, Bwana. Si kwamba kuna mtu yeyote anayestahili. Hatustahili, Bwana. Bali wewe uliahidi jambo hilo, na wakati huo umewadia. Neno linasimama mbele zetu. Tembea pamoja nasi, Bwana, usiku wa leo, na ufanye jambo fulani kama ulilofanya ulipokuwa duniani huko nyuma, miaka elfu mbili iliyopita, kusudi kanisa hili lipate kujua usiku huu ya kwamba U hai milele, ya kwamba ni Wewe yule jana, leo, na hata milele, na umeahidi kazi ulizofanya zitarudiwa tena. "Mwana wa Adamu atafunuliwa katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa huko Sodoma." Bwana, kamwe Wewe hukutaja hilo (kuhusu Lutu) kuhusu Nuhu. Hukutaja kamwe ya kwamba Wewe ungefunuliwa katika wakati wa Nuhu, bali ulisema, "Kama ilivyokuwa katika Sodoma, wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa." Loo, je . . .

126 Bwana, jalia wasomaji wa Biblia hapa usiku wa leo waone Ukweli. Jalia waone ya kwamba Malaki 4, ya kwamba upako huu unapaswa kuja, na kuirudisha tena Imani hiyo ambayo baba waliiona wakati mmoja, kule kufunuliwa kwa Mungu katika Kristo. Sasa jalia waone ufunuo wa Mungu katika wanadamu, Kristo akidhihirishwa katika mwili wa Kanisa Lake, akitembea miongoni mwetu. Tujalie, Bwana. Ahadi hizo ulizifanya, na ahadi hizo Wewe utatimiza. Nami ninajikabidhi, pamoja na

Neno, pamoja na kanisa, pamoja na wote, Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo.

127 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, je! kuna baadhi hapa, kabla hatujafanya mstari wa maombi, wangesema, "Ndugu Branham, mi—mimi si Mkristo. Ni—ni—ni—ninataka kuokoka. Niombee, utafanya hivyo, Ndugu Branham?" Inua tu mkono wako. "Nitafanya jambo hilo." Kama uko hapa tu, wala hu Mkristo. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mvulana. Mungu akubariki, bwana. Hilo ni zuri. Ninii tu. . . Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Mungu akubariki, huko nyuma, bwana. Mungu akubariki. Hilo ni jema.

128 Mtu mwingine inua tu mkono wako, useme, "Mimi si Mkristo"? Mungu akubariki. Nilikuona huko nyuma, kijana mwanamume. Mungu akubariki, huko nyuma kabisa. Na huku mbele kabisa pembeni, naam, Mungu akubariki. "Mimi si Mkristo, Ndugu Branham, bali ninaamini ya kwamba unasema Kweli. Ninaamini ni Kweli. Ninaamini ahadi inasema hivyo. Nimesoma, na ninaona ya kwamba ahadi iliahidi jambo hilo. Sijapata kuliona, bali ni—ni—ninaliamini." Mungu akubariki, msichana. Mwingine tu?

129 Unapoinua mkono wako, hilo linakufanyia jambo fulani. Hakika linakufanyia. Linakupa hisia kwamba umefanya jambo sahihi. Hakuna mtu wanaoweza kuinua mikono yao. . . Ninakuona, huko nyuma kabisa. Naam. Hakuna watu wanaoweza kuinua mikono yao ila. . . Mungu akubariki. Ninakuona pale, tena, na wewe hapa. Naam. Jamani, hilo ni zuri. Kumbuka, kama nisipouona mkono wako, Yeye anakuona. Anajua yote kuhusu jambo hilo. Kumbuka, Yeye anajua. Mungu akubariki, ewe dada mchanga. Yeye anajua jambo hilo.

130 Baba yetu wa Mbinguni, wao ni Wako sasa. Wasingeweza kuinua mkono huo; kuna kitu Fulani kilichowaambia wafanye hivyo. Na hata hivyo, labda, hakuna mmoja wao amewahi kuona ishara dhahiri za ajabu sana za Uwepo Wako hapa duniani katika siku za mwisho, bali wanauona hapa, Maandiko yalisema hivyo, na jalia wafahamu usiku wa leo. Ya kwamba, hata Biblia imehubiriwa kwa muda wa miaka hiyo yote, na, bado, watu hawaamini. Lakini wakati ulipompata Kleopa na rafiki yake, kisha ukageuka na kufanya jambo fulani jinsi hasa ulivyolifanya wakati ulipokuwa hai duniani kabla ya kusulubishwa, wao walijua kwamba huyo alikuwa ni Yesu yule yule. Sasa, Bwana, fanya jambo lilo hilo kwa ajili yetu usiku wa leo. Fanya, usiku wa leo, kwa ajili ya watu hawa wagonjwa, kama tu vile ulivyofanya kabla ya kusulubishwa Kwako; ndipo, baada ya miaka elfu mbili, wanaume na wanawake watajua ya kwamba Wewe U hai. Tunakungojea Wewe, Baba, kupitia Jina la Yesu. Amina.

131 Sasa kwenu ninyi mlioinua mikono yenu, ninawatakeni mketi kwa kicho sana kwa dakika chache. Nitaitisha mstari wa maombi. Sisemi ya kwamba Mungu atafanya jambo hilo. Bali ninataka kuwauliza swali zito, enyi watu. Kwa kuwa kuna, loo, mamia kadhaa hapa, ama mia tano ama mia sita, ama hesabu yoyote ile, angalieni, hao—hao ni watu wengi sana. Lakini, angalieni, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Sisi tunawajibika kwa Mungu. Tunawajibika. Naye anawajibika kwa ajili ya Neno Lake. Sasa kama Yeye akilifanya Neno hilo liishi tena, ninyi—nyinyi—nyinyi—ninyi . . . Ninataka kila mtu uliyeinua mkono wako, nawe ambaye hukuinua mkono wako, mara baadaye mje hapa msimame madhabahuni, mara tu tutakapowaombea wagonjwa.

132 Billy yuko wapi? Je! . . . Moja, kadi ya maombi D, moja mpaka mia moja? Vema. Hebu, tuna haraka, kwa hiyo tutaanza tu na namba moja. Kadi ya maombi D, namba moja, ni nani aliye nayo, inua mkono wako. Angalia kwenye kadi yako ya maombi, angalia ni gani. Kama huwezi kutembea, mbona, baadhi yenu shukeni mwende pale ili kwamba yeye . . . D, namba moja, mbili, tatu, nne, tano, simameni papa *hapa*, tafadhalini. Moja, mbili, tatu . . . Kama huwezi kutembea, inua mikono yako, nao watakubeba. Moja, mbili . . . Ninaona tu moja, hadi sasa. Naomba mje haraka, upesi tu mwezavyo, moja, mbili, tatu, nne, tano.

133 Kama mtu fulani angeweza kuzungumza katika Kihispaniola; ninaona kuna Wahispaniola wengi. D, moja, mbili, tatu, nne, tano. Moja, mbili, tatu . . . Vema, hao hapo watatu. Moja, mbili, tatu, nne, huyo hapo mwingine. Namba tano, ni nani aliye na kadi ya maombi namba tano? Inua mkono wako, mtu fulani. Ungesemaje katika Kihispaniola? Je! hiyo ni kadi ya maombi namba tano, bwana? [Mtu fulani anasema katika Kihispaniola, "Cinco."—Mh.] En-he? [Numero cinco, el numero cinco." "Hii hapa tano."] Hiyo hapo imepatikana. Asante. Moja, mbili, tatu, nne . . . Halafu, vema, ni ipi isiyopo? ["Zote zipo, tano."] Kuna tano hapo? ["Naam."] Naam, ninaona sasa. Sikumwona amesimama hapo nje. Vema.

134 Sita, saba, nane, tisa, kumi. Aisee . . . [Sehemu tupu kwenye kanda. Mtu fulani anasema katika Kihispaniola, "Seis, siete, ocho, nueve, diez."—Mh.] Sasa simameni hapa kwa muda kidogo tu. Sita, saba, saba, nane, tisa . . . Basi. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. ["Once, doce, trece, catorce, quince."] Hilo ni jema. Hilo ni safi. Hebu kidogo tu, hebu na tuwaite wengine zaidi. Kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini. Moja mpaka ishirini. Tuanze? Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa . . . kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane . . . Basi. Vema, hilo ni sawa. Hilo ni vema kabisa. Hebu na tuanze nao. Asante, ndugu.

135 Ni wangapi hapa wasio na kadi ya maombi, inua mkono wako, na hata hivyo wewe ni mgonjwa? Sasa kumbukeni, si lazima uwepo hapa juu. Haikulazimu kuwa hapa. Amini tu.

136 Sasa hebu kila mtu awe na kicho kabisa. Nitawaomba, katika Jina la Yesu, kwamba mtu yeyote asisogee kwa dakika zingine, kama kumi hivi, kumi na tano, dakika kumi ama kumi na tano. Hebu tu na—na—na tumpe Mungu heshima hiyo—hiyo kuu. Kila mtu na atulie kabisa. Hebu na tunyamaze kimya kabisa sasa. Hebu kidogo tu, naye atakuwa ameufanyiza mstari hapa. Sasa wakati yeye, wanapongojea pale, nisikilizeni kwa makini sasa.

137 Sasa je! mnatambua mahali ninaposimama hapa? Ni wangapi wanafahamu yale nimehubiri? Mnaona? Nami nimedai ya kwamba Yeye amefufuka katika wafu. Sasa amefufuka katika wafu, Naye aliahidi kufanya jambo hili. Sasa halijatukia katika miaka yoyote tangu mitume, mpaka wakati huu, kama tunavyojua, bali Yeye aliahidi kwa wakati huu, "Mwana wa Adamu atafunuliwa kama ilivyokuwa huko Sodoma." Sasa wewe soma jambo hilo katika Luka 17, kwenye 20 hadi 30, uone kama hiyo si kweli. Yeye aliahidi hilo.

138 Soma Malaki 4. Usiichanganye na Malaki 3, sasa. Malaki 3 ilikuwa ni Yohana Mbatizaji. Unaona? Lakini Malaki 4, mara jambo hili lilipokwisha, waov-. . . wenye haki wanatembea juu ya walio waovu, na ulimwengu ulichomwa kwa moto, unaona. Halikutukia siku za wakati wa Yohana. Tunatarajia upako huo mkuu juu ya Kanisa, ambao utaigeuza mioyo iyarudie Mafundisho asili ya baba zao, kuwarejesha kwenye pentekoste halisi na ya kweli.

139 Vema, iweni na kicho. Billy, sema kwa sauti kuu mara tu utakapowaweka wote kwenye mstari, hapo chini. Vema, nyote mko tayari? Sawa. Sasa, kwa kicho sana. Mtu fulani atasaidia, akitembea karibu. Sasa kila mtu na anyamaze kimya kabisa, kwa dakika chache tu.

140 Ninataka mnipe ahadi. Nilimwahidi Mungu ya kwamba nitaninii. . . Naye anajua moyo wangu na anaujua wako. Sasa, ninawajibika tu kusema jambo hili, lililo Kweli. Hayo ndiyo yote ninayowajibika kufanya. Mungu aliiandika; kamwe sikuiandika. Sio mimi, sio mimi; ni Biblia. Mnajua jambo hilo. Sasa kama Yeye atafunua jambo hilo, si hilo litamleta papa hapa akiwa hai miongoni mwetu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona?

141 Vipi kama hukuwa na hisi ya kuona, hakuna mtu aliyekuwa nayo, nawe ungetoka uende ukatembee kwenye jua. Wakati mwingine usingejua mahali ulipokuwa ukitembea, maana ulikuwa kipofu. Nawe ulitembea kwenye nuru ya jua, unasikia kitu halisi kimekuzunguka, chenye joto kweli, halafu baada ya kitambo kidogo ungeenda kutembea kwenye kivuli, nawe

ungesema, "Hakiko sasa." Hakuna mtu aliyepata kujua jua lilikuwa ni kitu gani, hujapata kuwa na hisi hiyo ya kuona, unaona, usingejua kilikuwa ni kitu gani.

Mtu fulani anasema, "Hiyo ni nuru ya jua."

142 "Nuru ya jua ni kitu gani? Nuru ni kitu gani, na jua ni nini?" Unaona, hujapata kusikia. Unaona?"

"Vema, ni nuru inayotoka juu."

"Nuru ni kitu gani?" Unaona?

143 Sasa hivyo ndivyo ilivyo. Tunahisi Uwepo wa Mungu, halafu, na hatuuhisi, kisha tunatembea katika Huo. Unaona? Nawe uko katika ki—kiwango ambapo unaona. Unaweza kusema ni Kitu gani. Unaona? Unajua Hicho ni nini.

144 Sasa, kama Mungu amefufuka katika wafu na yuko hapa usiku wa leo, Yeye aliahidi jambo hilo. Sasa umbo Lake la kimwili limekaa kwenye kiti cha Enzi cha Mungu; Yeye aliuchukua, akaketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Lakini Roho Mtakatifu yupo hapa, ambaye ni Kristo, katika umbo la Roho. Neno *Kristo* linamaanisha "Aliyetiwa mafuta." Na upako huo uliokuwa juu Yake, uko juu ya Kanisa, sisi sote. Sasa uliendelea tu kuja, kutoka katika kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurudishwa kwa vipawa, ukashuka moja kwa moja, mpaka kufikia kwenye kilele chake. Kweli. Linafikia uchache daima, liko pamoja sasa. Na sasa kuna kanisa, na sasa Bibi-arusi atatoka katika kanisa; unaona, kanisa litapitia kwenye wakati wa dhiki, sio Bibi-arusi. Samahani, sipaswi kuhubiri fundisho. Samahani. Vema.

Huyu ndiye yule bibi. Njoo hapa.

145 Angalia, siamini kuna mtu humu ndani ambaye ninamjua, ambaye ninamwangalia. Kama sifahamiani na kila mmoja wenu hapa, inueni mikono yenu, ninyi mnaojua sijui lolote kuwahusu; kwa hiyo hao watu ni wageni humu.

146 Sasa, tafadhalini, tafadhalini msisogee popote. Ketini kimya, mtafanya hivyo?

147 Wote walio kwenye mstari wa maombi, wasionijua mimi, na wanaojua sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu. Haya basi.

148 Sasa hili hapa kundi la wahudumu limeketi. Unaona, ni nje tu hapa ambapo sisi sote tunaweza kuangalia, unaona.

149 Sasa bibi huyu hapa ni mgeni kwangu. (Sasa yeyote aliye kwenye hiyo, mhandisi, angalia maikrofoni hiyo, sasa.) Vema, sasa nitamzungumzia. Hapa, hapa panajirudia, Yohana Mtakatifu 4, ambapo Yesu alizungumza na mwanamke fulani na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini, naye akaamini ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi wakati huo, ingali ni ishara ya Masihi,

maana ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Walikutana namna hii.

150 Sasa, mimi si Yesu, na bila shaka mwanamke huyu hapa si mwanamke wa aina ile. Lakini ninalojaribu kusema, ni vile vile; huyu hapa mwanamume akikutana na mwanamke, halafu kuna kitu kibaya hapo, na kama kitu fulani kitaingia hapa kufunua jambo hilo, hiyo inaonyesha haina budi kuwa ni Mungu. Sasa nisingejua, maana si—sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Mnaona? Naye aliinua mkono wake ya kwamba sikumjua, wala yeye hanijui, na sisi hawa hapa tumesimama tu.

151 Sasa ninataka tu kuzungumza nawe kwa dakika moja, baada ya mimi kuzungumza hivyo, kuhubiri, dada. Na kama hiyo . . . Kwa hiyo, unaona, mmoja anahubiri, mwingine anatia mafuta, kitu kingine.

152 Sasa kama Bwana Yesu angeweza kunielezea, ama kunionyesha kwa ono, jambo fulani unalotaka, jambo fulani ambalo labda huenda likawa ni ugonjwa, huenda likawa ni la kifedha, huenda likawa ni la kinyumbani, huenda likawa ni kwa ajili ya mtu mwingine. Hata sijui, unaona, sina fununu. Lakini kama Yeye angeniambia jambo fulani ambalo—ambalo ni kosa, ama jambo fulani ambalo ni kasoro maishani mwako, ama—ama jambo fulani, na ni kwamba wewe ni mgonjwa sana, ama mtu mwingine ni mgonjwa, ama kuna kasoro fulani. Kama angelisema, ungelijua kama ilikuwa ni kweli ama ni uongo. Wewe, unaweza kusema ni kweli ama la. Vema, kama Yeye anajua yaliyokuwako, basi hakika anajua yatakayokuwako. Kama anaweza kujua mambo yaliyopita, Yeye anaweza kujua mambo yaliyomo na ya usoni. Sasa je! lingekufanya uamini kwa moyo wako wote, ya kwamba ungepata unayoomba?

153 Je! Ingewafanya wasikilizaji kuamini ya kwamba wangepata Kile hii . . . ? . . . [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa msisogee kokote sasa. Ninangojea tu na nione, kuona kile Yeye angeniambia, maana sijui. Ninaninii tu, mkutano baada ya mkutano, ninashikwa na wasiwasi, mwajua, na kuhubiri, na kuharakisha, na kuangalia jambo *hili* na kile umeahidi, nami ninapaswa kuwatoa huko saa tatu u nusu; wakati huo umekaribia sasa; inanifanya kuwa na wasiwasi, kwa hiyo inanibidi tu kujituliza. Unaona? Ni ninii . . .

154 Kipawa si kitu kama vile unavyochukua kisu na kukata kitu fulani. Hicho si kipawa. Kipawa ni kujiondoa njiani ili Roho Mtakatifu apate kukutumia. Na hilo ndilo jambo pekee ninalopaswa kufanya, ni kumwondoa William Branham jukwaani, unaona, kusudi Mungu apate kuja.

155 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu Wake, kusudi Maneno ambayo nimehubiri yapate kudhihirishwa.

Yeye yupo hapa sasa. La—laiti ningaliweza kuwaambia jinsi ilivyo. Jamani, loo, jamani! Kama angeniambia ya kwamba kesho asubuhi niende kwenye makaburi ya Rais na kumfufua George Washington, ningewaambia mje mwangalie. Yale tu Yeye angesema sasa. Unaona? Sijui yale angesema, lakini, yale anayosema, yatakuwa ni kweli.

156 Bibi huyu anaugua maumivu ya macho yake. Ana shida ya macho yake. Yanamsumbua. Ana ugonjwa wa mgongo unaomsumbua. Ana wasiwasi, wasiwasi sana. Vema. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Tena, jambo jingine, wewe ni mhudumu wa namna fulani, wewe ni kama nanii mwanamke . . . Wewe ni mhubiri mwanamke. Hivyo ndivyo ilivyo. Sasa amini kwa moyo wako wote, nenda, nawe unaweza kupata ulichoomba.

Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

157 Njoo, bwana. Sisi hatufahamiani, nafikiri. Bwana anatujua sote wawili. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia? Sasa, huyo alikuwa ni mwanamke; huyu hapa mwanamume. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Ingekufanya uamini? Unaugua wasiwasi. Pia una shida ya macho yako; yanafifia wakati wote. Yamekuwa yakifanya hivyo kwa muda fulani. Jambo jingine, ninaona kitu fulani juu ya mkono wako. Loo, ni presha yako ya juu ya damu. Ni hiyo, wewe una presha ya juu ya damu. Hiyo ni kweli, sivyo? Vema, inua mkono wako kama mambo hayo ni kweli. [Huyo ndugu anasema, "Asante, Yesu!"—Mh.]

158 Kadiri unavyozidi kuzungumza na huyu mtu, ndivyo yangefunuliwa mengi, unaona. Sasa angalia, tazama, angalia. Shusha tu mkono wako. Hatuna wengi sana hapo; shusha tu mkono wako. Sasa, sijui yale niliyomwambia, bali yamerekodiwa pale, unaona, hivyo ndivyo yalivyo kwenye kanda. Sijui yale Yeye aliyosema.

159 Lakini hebu tuone sasa. Naam, ni macho, hilo ni jambo moja. Halafu basi, jambo jingine, una kuganda kwa damu na kuko huko kwenye ubongo, nawe ulipatwa na kiharusi. Hiyo ni kweli. Vema, unaamini sasa? Unaamini utapona? Unaamini huyo anayenena ni Mungu, sio mimi? Vema, basi nenda, amini. Hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya, ni kuamini tu. Kama wangeweza tu kuamini, hakuna lingine. Kama wakiamini tu, imekwisha.

160 U hali gani? Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, ninaamini."—Mh.] Na kama Yeye anaweza, je! itakufanya umwamini? ["Ndiyo."] Itakufanya uamini. Unaogopa nini? Hujui, sivyo? Ni kama kwamba ni giza tu, wasiwasi. Na halafu jambo jingine, una shida shingoni mwako. ["Ndiyo."] Hiyo ni kweli. Shida yako imo shingoni mwako. Halafu una mtu

fulani moyoni mwako, ambaye unamwombea. [“Ndiyo.”] Una shida nyingi sana na hilo. [“Ndiyo.”] Na hiyo ni juu ya pombe. [“Ndiyo.”] Ni mume wako. [“Ndiyo.”] Yeye ni mlevi sugu. [“Ndiyo.”] Nawe unamwombea. [“Ndiyo.”] Je! unaamini kwa ajili yake? [“Ndiyo, ninaamini.”] Basi nitaomba ya kwamba Yesu Kristo atakutendea mambo haya. Vema.

161 Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa hilo, kwa jumla, vema . . . Hao wawili, watatu, ama ninii, wanne, wowote wale ambao wamepita, idadi hiyo ni kama ile ya yale Yesu aliyofanya katika Biblia nzima. Unaona? Hiyo ni kweli. Yeye alimfanyia mwanamke fulani, akamwambia mwanamke huyo jambo hilo moja, Naye akashuka kwenda Sikari; Yeye hakumwambia mtu yeyote jambo moja zaidi kule chini, bali waliamini kwa ajili ya ushuhuda wa mwanamke huyo. Naam. Haimbidi mwanamke huyo kukushuhudia; umesimama papa hapa ukiliangalia, wewe mwenyewe. Inakubidi tu kuamini. Maana, wengine wasingeamini, hakuna kitu ndani yao cha kuaminia.

162 U hali gani? Sasa, hatufahamiani. Hivi si ningekuwa mtu mbaya sana nikisimama hapa kama . . . Mwanamke mzuri sana mwenye nywele za mvi namna hiyo, na kuwazia mambo, na mama yangu wa thamani angalikuwa na umri kama huo, naye ndiyo kwanza aage dunia hapa miaka michache iliyopita. Na kukiwako na jambo lolote ninaloweza kufanya kumsaidia maskini bibi huyo, nitalifanya. Ninajua, kama—kama yeye ni mgonjwa, kama ningeweza kuchukua na—na kusukuma sarafu kwa pua langu kuzunguka mji huu, ningefanya hivyo. Sijali ni nani angenicheka. Ni—ninataka apone. Kama ningeweza kumsaidia, ningefanya hivyo. Lakini siwezi kumsaidia. Na kadiri Yeye alivyofanya, Mungu alikuwa amefanya hivyo tayari. Naye anakupenda kuliko ninavyokupenda. Alikufa kwa ajili yako; wala mimi sikufanya hivyo. Lakini Yeye alikupenda vya kutosha kukufia.

163 Lakini basi Yeye alinitumia kipawa kidogo tu. Alimtuma mchungaji wenu hapa kuomba na kuwawekea wagonjwa mikono, na, unaona, hilo limefanywa sana katika ufufuo, kwamba hilo kwa namna fulani liko katika siku zilizopita, mwajua. Na sasa liko kwenye zingine, mnajua yale ninayomaanisha, kwa jumla, kitu kingine.

164 Sasa kama Bwana atanifunulia shida yako ni nini, je! unaamini kwamba mimi ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Unaamini kwamba ni Yeye? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, ninajua hilo.”—Mh.] Wewe, wewe, vema, ninakushukuru, dada. [“Hakika.”] Sasa ninaamini shida hiyo ya figo ambayo imekuwa ikikusumbua itakuacha. Je! unaamini jambo hilo, pia? Una ombi moyoni mwako, unalotaka kuniomba. [“Ndiyo.”] Vipi kama nikifunua ombi hilo kabla hujaniomba, je! ungeninii, ingekufanya uzidi kuamini? [“Hakika.”] Unataka nimwombee

binti yako. Yeye hayupo hapa. Hiyo ni kweli. Je! unataka nifunue shida yake ni nini? Ni wasiwasi kwelikweli. Sasa amini, naye atapona. Unaona? Mungu akubariki, dada.

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Unaona?

165 Neno la Mungu hufanya nini . . . Angalia kama wahudumu hawa hawasemi jambo hili. Biblia ilisema, katika Waebrania, Agano Jipya, mlango wa 4, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hutenganisha, hata mafuta ya mfupa, na huyatambua mawazo, makusudi ya moyo." Hiyo ni kweli, ndugu? [Wahudumu wanasema, "Amina."—Mh.] Unaona?

166 Ni kitu gani? Ni Neno lililogawiwa kwa ajili ya siku hii. Neno lililogawiwa kwa ajili ya siku hii, likitimiza ahadi hii, "Wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa, siku za Sodoma, mambo haya mengine yote yaliyoahidiwa," haya hapa, ni Neno la Mungu likifunuliwa, maana ni Neno Lenyewe likiyatambua mawazo yaliyo moyoni. Unaona? Hiyo ni kweli kabisa.

167 Sasa, mama huyu, simjui, mtu mwingine anayeonekana mpole. Ningekuwa nini, mtu mbaya sana, kama ningeweza kusaidia na . . .

168 Sasa hebu kidogo tu. Mtu mwingine, ilikuwa ni mwanamume fulani, ilikuwa ni mwanamume ndiye aliyetokea, na mtu mwingine huko nje akiomba. Iweni tu na imani. Ni—ninaona sasa ni . . . Itanibidi tu kusema ninachoangalia. Unaona, hivyo tu ndivyo ninavyoweza kusema, ni kile—kile ninachoona.

169 Wewe unaninii, ndiyo, unaumwa ugonjwa wa tumbo. Uko kwenye tumbo lako. Tena unataka kuniomba jambo fulani, na hilo ni kwa ajili ya mama yako. Hayuko hapa, bali ni mgonjwa. Unataka nimwombee. Sivyo? Una ombi lingine. Ni kwa ajili ya . . . Ni mtu fulani asiye hapa. Ni mbali na hapa. Na ninaona ni mbali . . . Ni katika nchi nyingine. Ni mbali sana na hapa. Na ni—ni kijana, mtoto anayeugua namna fulani ya ugonjwa, ugonjwa wa tropiki. Marekani ya Kusini, hiyo ni kweli kabisa. Liko juu yako. Hiyo ni kweli kabisa. Kweli. Lakini amini kwa moyo wako wote sasa.

170 Mimi siponyi. Yeye tayari ameponya. Hivi huwezi kutambua huo ni Uwepo Wake tena? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Itanibidi kuendelea na kuendelea tu, sasa limeanza kunipofusha kidogo, mnaona.

Mnasema, "Hiyo?"

171 Vema, ndugu, dada! Yesu, mwanamke aligusa vazi Lake, Yeye akageuka na kuona ilikuwa ni kitu gani, ndipo akasema, "Nguvu zimenitoka." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Vema, Yeye alikuwa, huyo alikuwa ni Mungu. Na mimi je, mwenye dhambi? Huna budi kuamini. Usitie shaka. Amini. Hii ni . . .

172 Je! unaamini? Msichana, nawe unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia kwamba shida yako ni nini? Vema, je! waweza, je! utakubali na kuamini kwa ninii wako wote... Unajua ingekuwa ni kweli. Unaona? Sasa jambo moja ambalo ndilo shida yako, ni mgongo wako, unaumwa na mgongo. Halafu una shauku kubwa moyoni mwako, ya jambo fulani, na, hiyo ni, unautafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli kabisa. Unaamini jambo hilo? Vema, utaupokea. Amina. Sasa nenda ukaamini kwa moyo wako wote, nawe utaupokea ubatizo huo.

173 Je! unaamini Mungu anaweza kuponya yabisi hiyo kavu na kukufanya mzima? Sasa, endelea tu kutembea na kumshukuru. Hiyo ni kweli, sasa. Unaona? Kama utaamini tu! Vema, bwana.

174 Waweza kuja, mama, jinsi tu ulivyokuwa umeketi pale, tafadhali. Je! utakuja? Unaamini kwa moyo wako wote? [Huyo dada anasema, "Ninawezaje kulitilia shaka?"—Mh.] Sasa, hiyo ndiyo njia, basi hutakuwa na yabisi kavu. Haitakulemaza. Nenda zako tu, na ukishangilia. Shida hiyo ya akina mama inakoma, pia. Nenda zako tu, ukimshukuru Bwana, ukisema—ukisema, "Mungu asifiwe!" Vema. Vema.

175 Sasa wewe amini unayeketi hapo, mama, je, unaamini? Vema, bwana. Sasa hiyo shida ya akina mama ambayo umekuwa nayo, shida ya akina mama, kwa muda mrefu; amini tu kwa moyo wako wote, na uende na itakuwa...utapona, wala hutakuwa nayo tena, kama utaamini jambo hilo. Inakupasa kuamini.

176 Vema, mleteni mama huyo, msichana huyo mdogo. Njoo hapa, kipenzi. Sasa, dada, hapa, nitaushika mkono wake, kwa muda kidogo tu. Njoo hapa, kipenzi. Nilifikiri hivyo ndivyo ilivyokuwa. Mara nyingi unasongwa roho, sivyo, huwezi kupumua, ni vigumu? Maskini pumu hiyo ya kale ni mbaya sana, bali Mungu anaweza kuiponya. Hivi huamini hilo?

Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya mtoto huyu...?...

177 Usitilie shaka, dada. Itamwacha. Nenda na ukaamini sasa, kwa moyo wako wote.

178 Mungu huponya kisukari. Yeye anaweza kuponya chochote atakacho. Huamini hilo? [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Je! unaamini ya kwamba atakuponya? ["Amina."] Vema, sema, "Asante, Bwana," na uende zako moja kwa moja, ukishangilia tu.

179 Hebu kidogo. Ninafululiza tu kuona mwamume akija hapa, kumbe. Hili hapa. Maskini jamaa mdogo anayeketi pale, amemshika mvulana mdogo mikononi mwake. Je! unaamini, bwana? Hunijui mimi. Je! unaamini Mungu anaweza kunifunulia unachohitaji? Unaona, ulimgusa Yeye. Sikujui. Lakini unaugua ugonjwa fulani, ugonjwa wa mfupa. Hiyo ni kweli. Maskini mvulana wako hapo anao. Mvulana wako mdogo anayeketi karibu naye anao. Huyo ni msichana wako mdogo anayeketi karibu na huyo. Yeye, ni katika mikono yake, naye ana

makengeza. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa je! unaamini? Usitilie shaka. Mwamini Mungu. Usitilie shaka kamwe. Amini tu. Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.

180 Kwa nini unalia, maskini mama, unayeketi pale, hapo mwishoni, uliyefunika uso wako kwa leso, ukilia? Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia kuwa shida yako ni nini, kutoka hapa? Una shida ya kiroho unayoiwazia. Sivyo? Yote itakwisha. Itakuwa sawa.

181 Bibi huyo anayeketi karibu nawe hapo, ndiyo kwanza uzungumze naye muda kidogo. Ndiyo kwanza aufunike uso wake kwa leso. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini, dada? Je! utaniamini, kama nabii Wake, mtumishi Wake? Utaniamini? Vema. Ugonjwa huo wa uvimbe puani ambao umekuwa ukikusumbua, utakuacha kama utaamini jambo hilo. Je! utaamini? Kama utaamini, inua mkono wako, useme, "Ninaamini."

182 Unataka kula chakula chako cha jioni, kutokana na ugonjwa huo wa tumbo, karibu na hapa, mama. Je! unaamini kwa moyo wako wote, pia?

183 Bibi anayefuata ana matatizo ya kiroho pale. Nawe una vipele, pia, vinavyokusumbua. Una binti aliye na vipele, pia. Je! si hiyo ni kweli? Naam, bwana. Ameketi ndani. Je! unaamini jambo hilo? Vema, unaweza kuponywa kama unaamini.

184 Vipi upande *huu*? Hapa, mnamwona maskini mwanamume huyu, wa Kimeksiko anayeketi hapa mwishoni, anayeniangalia moja kwa moja? Hivi hamwioni ile Nuru inayoning'inia juu yake? Juu ya mwanamume huyo ni giza, mnaona, kinachomzunguka, hicho ni kifafa. Je! unaamini Mungu anaweza kukuponya kifafa, bwana? Unaamini? Vema, Yeye atakuponya.

185 Mwingine, maskini mwanamume huyo aliye karibu nawe hapo, maskini, mwanamume Mhispaniola, yeye ana henia. Je! unaamini Mungu anaweza kuponya henia yako, bwana? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Unaamini?

186 Mwingine, anaumwa na tumbo. Wewe ambaye unatikisa kichwa chako hapo, unaumwa na tumbo. Je! unaamini Mungu alikuponya? Basi nenda ukale chakula chako cha jioni, atafanya hivyo.

187 Niambieni wanagusa kitu gani, huko kote kwa wasikilizaji. Ni kitu gani? Ni dhihirisho la Neno la Mungu. Je! mnaamini hilo, ninyi wenyewe? Mnaamini? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

188 Wako wapi wengine wao hapa? Hapa, huyu hapa mtu amelala kwenye machela. Bwana, sikujui mimi. Sijapata kukuona. Je! unaniamini mimi? Je! unaamini yale umesikia ni Kweli? Unaamini kwa moyo wako wote? Kama—kama Mungu

angeniambia hapa una shida gani, uta—utaninii . . . ungeamini? Nitakwambia jambo fulani sasa. Nawe unalijua, unayeketi karibu naye. Yeye ametiwa uvuli wa mauti. Ni kansa. Ni kansa. Nawe ni mhudumu wa Injili. Ninakuona umesimama mimbarani. Na hiyo ni kweli. Nawe umetokea nje ya mji. Sasa amini kwa moyo wako wote. Amini kwa moyo wako wote. Kwa nini ulale hapo mpaka ufe? Unaona? Huwezi kupata hasara.

189 Kulikuwako na watu kadhaa wenye ukoma. Je! unakumbuka hadithi hiyo, wakati Samaria ilipozingirwa, hao wenye ukoma waliingia mle? Wakasema, "Kwa nini tuketi hapa mpaka tufe? Kama tukiketi hapa, tunakufa; kama tukiingia mjini, tunakufa."

190 Daktari amefanya yote awezayo kufanya. Hakuna kitu kinachoweza kufanywa, ndilo jibu lake kwa jambo hilo. Una nafasi moja tu. Hao wenye ukoma walikuwa na nafasi mara moja, kama walishuka wakaenda kwenye nyumba ya adui; kama waliwaokoa, waliishi; kama hawakuwaokoa, wangekufa, haidhuru. Bali wewe huombwi kuingia katika nyumba ya adui. Uko mbele za Mungu wako. Unatarajia kuninii . . . Kwa nini usisimame, na kuchukua machela hiyo uende nyumbani, katika Jina la Yesu Kristo. Na uamini, na uende nyumbani na kuamini umeponywa.

191 Je! ninyi wengine mtaamini jambo lilo hilo? Kama mnaamini, simameni kwa miguu yenu.

192 Ninawaomba hao watu walioinua mikono yao, kama walitaka kuokoka, na walitaka kumkubali Yesu Kristo, ninawataka mje hapa na kusimama hapa karibu nami, kwa dakika moja tu. Je! mtakuja sasa? Njoni hapa, ninyi mlioamini na mnataka kumkubali Kristo. Kamwe hamtakuwa karibu zaidi Naye mpaka mtakapokutana Naye katika mwili. Kumbukeni, hilo Neno, nami nimehubiri, Mungu amelithibitisha kuwa ni Kweli. Njoni, njoni *huku*, kila mmoja wenu. Kila mtu ambaye hakumjua Kristo, mlioinua mikono yenu, basi mje hapa; tuseme mlikuwa wenye dhambi, nanyi mlitaka kuokoka, njoni hapa mkasimame kwa dakika moja, kwa ajili ya maombi. Mtafanya hivyo? Mtakuja wakati Yeye akiwa karibu sana jinsi hiyo?

193 Unamaanisha ungeweza kuona Neno hapa likihubiriwa, umwone Mungu akigeuka na kusema ya kwamba Neno hilo ni Kweli, "Huyo ni Mimi, huyo ni Mimi, ninasimama hapa, Mungu yule yule atakayekuhukumu," kisha usitesite? Usifanye hivyo, huenda ukajikatilia mbali milele. Unaona? Hawa hapa watatu wamesimama hapa. Kuna yapata dazani mbili. Njoni sasa hivi, mtakuja?

194 La, hakuna wimbo, si lazima uwe na wimbo. Kristo ndiye wimbo wako. Kristo ndiye imani yako. Neno ndilo linalosema hivyo.

195 Hiyo ni kweli, hawa hapa wavulana wawili wanakuja. Njoni moja kwa moja, ninyi mlio wenye dhambi. Shukeni mje papa

hapa kwa muda mfupi tu, mtakuja? Moja kwa moja wakati ninaposikia kuongozwa, nilisimamisha mstari huo wa maombi kwa kusudi hili. Njoni papa hapa sasa. Njoni papa hapa. Tutaufikia mstari wa maombi. Ninii tu . . . Hiyo ni kweli. Naam, enyi akina mama njoni moja kwa moja *hapa*, wasichana.

196 Moja kwa moja katika siku hizi wakati vijana hawa wanapokuja, katika saa hii iliyo kuu wakati kungali kuna matineja waliozama katika utovu wa uadilifu, watu hawa wanakuja kuninii . . . Nami ninatumaini ya kwamba Mungu atawafanya mifano mizuri sana hivi kwamba mpaka, kwenye ujirani, ambapo watu wataona kwamba Yesu Kristo angali anawaokoa waliopotea.

197 Hivi hamji? Njoni moja kwa moja, mahali mlipo. Shukeni mje hapa chini, kwa muda kidogo tu. Hiyo ni kweli. Mungu awabariki, enyi wavulana. Hilo ni zuri. Njoni moja kwa moja huku mkasimame. Njoni, njoni. Huko nyuma nyuma kabisa, watu fulani huko nyuma kabisa mliinua mikono yenu, si mshuke mje huku chini sasa?

198 Karibu ninawashawishi. Nina . . . [Ndugu Branham anaanza kugonga mimbara—Mh.] Neno anasimama nje, akibisha, akijaribu kuingia. "Tazama, nasimama mlangoni, nikibisha; kama mtu yeyote atafungua na kuingia, kuniruhusu niingie, nitakula pamoja naye, naye pamoja Nami." Mbona usije? Shuka uje moja kwa moja sasa, usimame hapa. Angalia, Neno limehubiriwa, limethibitishwa, Kristo amefufuka katika wafu, Huyu hapa akifanya tu yale alisema Yeye angefanya. Hajajiunga na mashirika, madhehebu, apate kukuingiza ndani ya kitu fulani; hilo ni chaguo lako. Ninakutaka umchukue Kristo sasa.

199 Njoo, hivi hutakuja? Yupo mwingine? Ni . . . Mungu akubariki. Hiyo ni kweli, mlete moja kwa moja huku juu.

200 Ndugu, mtakuja hapa chini? Sasa hawa watakuwa washiriki wa makanisa yenu. Njoni huku chini.

201 Njoni, mtu mwingine. Moja kwa moja Mbele za Kristo, ninaweza tu kusikia Roho akiita moyoni mwangu. Hakika, kama hilo linafanya hivyo moyoni mwangu, kuna mtu fulani huko nje anayepaswa kuja. Je! yupo mtu aliyerudi nyuma huko nje ambaye anapaswa kuja? Njoo, simama hapa. Mtakuja, baadhi yenu? Uliyerudi nyuma, utakuja? Hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Njoo huku. Jambo ndilo hilo, shuka uje moja kwa moja. Hakika. Ndivyo hivyo. Kuwa mwanamume halisi; mama halisi. Mungu alikufanya, mama wa heshima. Mungu alikufanya, mwanamume. Huo ni uadilifu. Hizo ni nguvu. Njoo sasa, je! hutakuja? Njoo, simama hapa karibu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Mungu anakutaka katika Uwepo Wake wa Kiungu. Kumbukeni, ninii hasa . . .

202 Mungu atauhukumu ulimwengu kwa Nani? Yesu Kristo. Ni nani aliyeahidiwa kufanya jambo hili katika siku za mwisho,

kujifunua Mwenyewe? Yesu Kristo. Sio mimi. Ni Kristo. Kristo Ndiye aliye hapa akijifunua Mwenyewe. Unyenyekevu, kama alivyokuwa; akitoka mahali duni kabisa, kama alivyofanya; akiingia ndani yetu, kama vile amefanya. Yeye ni Mungu.

203 Sasa kila mmoja wenu wahudumu kusanyikeni huku chini mkiwazunguka watu hawa, upesi sana sasa shukeni mje miongoni mwao hapa, simameni moja kwa moja mkiwazunguka. Tutawaombea.

204 Kuna mtu mwingine anayetaka kuja katika maombi haya? Hebu kidogo tu. Sawa.

205 Hawa watakuwa washiriki wa makanisa yenu, enyi marafiki. Hii itakuwa...Ninyi, itawabidi kuwachukua tangu hapa na kuendelea, sasa. Wanamwona Bwana Yesu katika nguvu Zake za kufufuka Kwake. Wako hapa wapate kuwa washiriki wa kanisa lako. Wewe wabatize katika ubatizo wa Kikristo, wachukueni muwapeleke kwenye ushirika wenu. Ni wako sasa, tangu sasa na kuendelea. Wewe ndiwe mwangalizi katika nyumba ya wageni.

206 Na tuinamishe vichwa vyetu, kila mtu. Kila mtu, Mkristo aliye huko nje, ambaye ni mwaminifu, waombee watu hawa.

207 Na endapo wahudumu hawa wanataka kuwaingiza chumbani, ambamo wanaweza kufunzwa zaidi, ni sawa.

208 Baba wa Mbinguni, haya ndiyo matokeo ya mkutano huu. Hawa hapa wenye dhambi wanakuja, kumi na watano ama ishirini wamekusanyika hapa madhabahuni, wakitaka kukupa Wewe mioyo yao. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawapokea, katika Jina la Kristo Yesu Bwana. Ninaomba kwamba utawapokea, uwape Uzima wa Milele. Wao ni urithi Wako, Bwana.

209 Kila mtu humu ndani, ambaye ni mgonjwa sasa, wekeaneni mikono. Nyosheni mikono, wekeaneni mikono, na muanze kuomba, mmoja kwa mwingine. Wekeaneni mikono, muanze kuomba, mmoja kwa mwingine.

210 Wahudumu, wekeni mikono yenu juu ya watu hawa hapa. Naam. Kuna nguvu na utukufu na baraka juu yetu, na Shetani ameshindwa Mbele za Kristo.

Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua SWA64-0212
(When Their Eyes Were Opened, They Knew Him)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 12 Februari, 1964 katika Ukumbi wa Mikutano wa Elliott huko Tulare, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org